# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA UJENZI

# MCHANGO NA UMUHIMU WA SEKTA YA UJENZI KWA MAENDELEO YA UCHUMI NA USTAWI WA MAISHA YA WANANCHI

# YALIYOMO

1. UTANGULIZI – SEKTA YA UJENZI NI NINI
2. MCHANGO KATIKA UCHUMI
3. MCHANGO KATIKA MAENDELEO YA JAMII
4. SEKTA YA UJENZI NA DIRA 2050



# UTANGULIZI - SEKTA YA UJENZI

- inahusika na ujenzi wa miundombinu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.
- hujumuisha hatua na taratibu zinazowezesha ujenzi wa miundombinu:
  - kuandaa mipango ya ujenzi,
  - usanifu,
  - ununuzi,
  - ujenzi,
  - matengenezo,
  - ukarabati na
  - ubomoaji.



# UTANGULIZI – SEKTA YA UJENZI…2

- Miundombinu inayojengwa ni pamoja na:
  - majengo,
  - barabara,
  - reli,
  - bandari,
  - viwanja vya ndege,
  - madaraja,
  - mabomba ya kusafirishia mafuta, maji na gesi,
  - njia za umeme,
  - mifumo ya maji safi na majitaka,
  - mabwawa,
  - mifumo ya umwagiliaji,
  - njia za maji,
  - nishati,
  - mahandaki, na
  - migodi.





# UTANGULIZI-SEKTA YA UJENZI…3

- Utekelezaji wa miradi unahusisha wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa ujenzi.
  - kampuni, taasisi au mtu mmoja mmoja.
  - taasisi za udhibiti,
  - makandarasi,
  - washauri elekezi,
  - wazalishaji wa vifaa na mitambo ya ujenzi,
  - wasambazaji wa vifaa na mitambo ya ujenzi,
  - mafundi ujenzi,
  - na watoa huduma mbalimbali katika miradi ya ujenzi (benki, bima, ulinzi, vyuo vya mafunzo, n.k.).



# UTANGULIZI-SEKTA YA UJENZI…4

- Kimsingi sekta ya ujenzi ni sekta wezeshi kwa sekta nyingine za kiuchumi na kijamii,
  - hujenga miundombinu inayotumiwa na sekta nyingine kwa ajili ya uzalishaji au utoaji huduma za kijamii.
- Manufaa yake ni pamoja na
  - kutoa ajira,
  - kujenga miundombinu mbalimbali inayotumika katika shughuli za kijamii na kiuchumi,
  - huchangia katika pato la taifa,
  - Kukuza maarifa, ujuzi na teknolojia, na
  - utunzaji wa mazingira.



# WADAU WA SEKTA YA UJENZI

**BIASHARA YA VIFAA NA MITAMBO YA UJENZI**

- Vifaa vya ujenzi (raw materials supply)
- Viwanda (Processing and manufacturing)
- Usafirishaji (Material and equipment distribution)
- Mitambo (equipment rental and leasing)
- Kurejelezea (recovery and recycling)

**HUDUMA ZA KITAALAM**

- Huduma za ubunifu majengo (Architecture services)
- Huduma za ukadiriaji majenzi (Quantity surveying)
- Huduma za kihandisi (Engineering and technical services
- Uendelazaji milki (property development)
- Matengenezo na ukarabati (building maintenance)
- Kupangisha (building occupation)
- Menejimenti ya milki (property management)

**UJENZI**

- Mkandarasi mkuu (main contractor)
- Makandarasi maalum (installation specialists)
- Usimamizi wa miradi (project management)
- Uvunjaji na menejimenti ya masalia (demolition and waste management)

**HUDUMA NYINGINE**


- Huduma saidizi: Huduma za kifedha, sheria, huduma za maarifa na ufundi, ujuzi na mafunzo
- Sekta zinazo husiana: nishati, maji, mawasiliano, ugavi na usafirishaji, usafi, na ulinzi
- Taasisi simamizi za sekta, vyama vya kutetea maslahi ya wadau

# SEKTA YA UJENZI NA PATO LA TAIFA (GDP)





- Umuhimu wa Sekta ya ujenzi kwenye uchumi wa nchi hupimwa kupitia mchango wake kwenye
  - pato la Taifa (Gross Domestic Product - GDP),
  - kutoa ajira, na
  - mchango wake katika rasilimali za kudumu za Taifa (Gross Fixed Capital Formation - GFCF).
- Wastani wa mchango wa sekta ya ujenzi katika pato la Taifa (GDP) nchini kwa kipindi cha miaka saba (2018 – 2024) ni **asilimia 13.5**
  - *(Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2024).*

# SEKTA YA UJENZI NA PATO LA TAIFA (GDP)…2





- *Mchanganuo wa mchango Pato la Taifa Kisekta kwa Mwaka 2024 (NBS, 2024)*

# SEKTA YA UJENZI NA PATO LA TAIFA (GDP)…3





***Mchanganuo wa Pato la Sekta ya Ujenzi kwa Bei za Miaka Husika (Shilingi Milion) (NBS, 2024)***

# SEKTA YA UJENZI NA AJIRA




- Mchango wa sekta ya ujenzi kwenye ajira ulifikia **asilimia 3.5,** ukichangia jumla ya ajira **872,582.34** kati ya ajira rasmi **24,930,924** zilizopatikana mwaka 2024 (NBS, 2024).

# SEKTA YA UJENZI NA AJIRA…2




- *Mchanguo wa Ajira Kisekta mwaka 2022/2023*

  *(NBS, 2024)*

# MCHANGO WA SEKTA YA UJENZI… BENKI

- Inakadiriwa **asilimia 19.6** ya mikopo yote iliyochukuliwa katika taasisi za fedha kwa mwaka 2024 ilikuwa kwa madhumuni ya ujenzi wa nyumba na ununuzi wa viwanja.
- mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 1.98** imetolewa kwa watumishi wa Serikali kupitia Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali,
- mikopo ya **shilingi bilioni 659.3** kupitia taasisi za fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.
- Taasisi za Fedha na Benki zinazotoa huduma za mikopo ya ujenzi wa nyumba zimefikia 31



# SEKTA YA UJENZI NA ELIMU (AWALI NA SEKONDARI)

- Kuimarisha miundombinu ya elimu
  - kujenga shule 26 za Kitaifa za sayansi za wasichana kwa kila mkoa na shule 7 za wavulana kila kanda;
  - kuongeza vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari kutoka madarasa 191,708 mwaka 2020 hadi madarasa 254,393 mwaka 2025;
  - kuboresha shule 274 za michepuo ya kilimo na shule 28 za michepuo ya biashara;
  - kujenga shule za sekondari 1,031, kutoka 3,863 hadi shule 4,894 mwaka 2025;
  - kujenga shule mpya za msingi kutoka 16,406 mwaka 2020 hadi 17,986 mwaka 2025;
  - kuongeza nyumba za walimu kutoka 58,637 mwaka 2020 hadi 60,429 mwaka 2025;
  - maabara 8,072 mwaka 2020 hadi 8,710 mwaka 2025;
  - maktaba 1,537 mwaka 2020 hadi 2,665 mwaka 2025;
  - mabwalo 871 mwaka2020 hadi 1,004 mwaka 2025;
  - kukamilisha ukarabati wa shule za sekondari 74 na shule za msingi 794 pamoja na kuendelea na ujenzi wa shule 29 za amali za mikoa.



# SEKTA YA UJENZI NA ELIMU (Elimu ya Ualimu)

- Kujenga vyuo vya Ualimu vya Sumbawanga, Dakawa, Mhonda, Kabanga na Ngorongoro;
- Kujenga miundombinu ya madarasa 41, kumbi za mihadhara tatu (3) na mabweni 15 katika vyuo 23 vya ualimu
- kukarabati miundombinu katika Vyuo vya Ualimu vya Songea, Tarime, Mamire, Katoke, Singachini, Vikindu, Bunda, Mtwara (Ufundi), Mtwara (Kawaida), Monduli, Bustani, Butimba, Kasulu, Kleruu, Patandi, Mpwapwa, Korogwe na Morogoro.



**Chuo cha Ualimu Kabanga, Kasulu**

# SEKTA YA UJENZI NA ELIMU (Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi)

- Ujenzi wa vyuo 29 vya mafunzo ya ufundi stadi ambavyo vimeanza kutoa mafunzo pamoja

- kuendelea na ujenzi wa vyuo 65

- Kukamilisha ukarabati wa vyuo 10 vya VETA vya Ileje, Urambo, Nkasi, Newala, Muleba, Itilima, Babati, Kilindi, Ngorongoro na Kasulu; na

- Ukarabati wa vyuo sita (6) vya ufundi stadi na huduma za utengano wa Watu Wenye Ulemavu katika mikoa ya Tanga (Masiwani), Tabora (Luanzari), Singida (Sabasaba), Dar es Salaam (Yombo) na Mtwara (Mtapika).




**Igunga DVTC**

# SEKTA YA UJENZI KATIKA SEKTA YA AFYA

- Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025
  - kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 8,783 mwaka 2020 na hadi 12,846 mwaka 2025 sawa na ongezeko la vituo 4,063
    - Zahanati zimeongezeka kutoka 7,242 hadi 8,328;
    - Vituo vya Afya kutoka 1,205 hadi 1,254;
    - Hospitali zenye hadhi ya ngazi ya Wilaya kutoka 148 hadi 361;
    - Hospitali zenye hadhi ya Mkoa kutoka 23 hadi 76;
    - Hospitali zenye hadhi ya Kanda 18; Hospitali Maalumu 6.
  - Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali za Kanda ya Kusini Mtwara na Chato.
  - majengo mapya yamejengwa katika
    - Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini - KCMC
    - Hospitali ya Kanda Mbeya na Hospitali ya Benjamin Mkapa - Dodoma (Jengo la kutolea huduma za Saratani) na
    - Hospitali ya Kanda ya Bugando (Wodi ya wagonjwa wa Saratani);




**Muhimbili - Mloganzila**

# SEKTA YA UJENZI KATIKA SEKTA YA AFYA…2

- Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Katavi, Njombe, Songwe, Simiyu, Geita, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mara na Lindi.
- Kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa majengo mapya ya kutolea huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Mtwara (Ligula), Mwanza (Sekoutoure), Kigoma (Maweni), Rukwa (Sumbawanga), Tabora (Kitete) na Mwanza (Ukerewe);
- Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali mpya 135 za Halmashauri, Vituo vya Afya 390, maboma ya Zahanati 980.
- Ujenzi wa nyumba za Watumishi 270 na
- ukarabati wa Hospitali Kongwe 50 za Halmashauri.
- Kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya kutoa huduma za afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda-Meta iliyopo katika Jiji la Mbeya na
- Hospitali za Rufaa za Mikoa ambazo ni Sekou Toure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe.



**Hospitali ya Rufaa ya Kanda-Meta**

# SEKTA YA UJENZI NA SEKTA YA MAJI




- Kutekeleza jumla ya miradi **2,331** ya usambazaji wa maji mijini na vijijini. Baadhi ya miradi kielelezo katika hii ni:
- Mradi wa majisafi na usafi wa mazingira Arusha uliogharimu zaidi ya shilingi bilioni **520**.
- Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Miji ya Tinde na Shelui kwa gharama ya shilingi bilioni 24.75.
- Mradi wa Maji Same – Mwanga - Korogwe ambao umeanza kutoa huduma ya maji katika Miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 43 vya Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe
- Mradi wa Maji wa Mugango – Kiabakari – Butiama kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 30.69.
- Mradi wa maji wa Orkesumet kwa gharama ya shilingi bilioni 38.11
- Mradi wa uchimbaji wa visima 1,749 na mabwawa 16 kwa ajili ya kutoa huduma ya maji katika maeneo mbalimbali nchini;

# SEKTA YA UJENZI NA SEKTA YA MAJI…2



**SAME – MWANGA - KOROGWE**

# SEKTA YA UJENZI NA SEKTA YA MAJI…3



- Ujenzi wa Bwawa la Kidunda linalogharimu Shilingi bilioni 329.47 kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani

  Ujenzi wa mradi wa maji wa Tunduma - Vwawa kwa gharama ya shilingi bilioni 119.95

  Ujenzi wa Mradi wa Maji Ruangwa, Lindi hadi Nachingwea wenye thamani ya Shilingi bilioni 107

  Ujenzi wa mradi wa maji kutoka Kahama kwenda Halmashauri ya Ushetu wenye thamani ya Shilingi bilioni 42

  Ujenzi wa mradi wa maji kutoka Dambia kwenda Hydom Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu wenye thamani ya Shilingi bilioni 41 na

  Ujenzi wa Mradi wa Maji Ukirigulu, Koromije hadi Sumve wenye thamani ya Shilingi bilioni 32.

# SEKTA YA UJENZI NA VIWANDA



- Kuanzishwa jumla ya viwanda 47,063 kwa kipindi cha miaka mitano yaani mwaka 2020 hadi 2025.

# SEKTA YA UJENZI NA KILIMO NA UMWAGILIAJI



- Kuongeza kwa eneo la umwagiliaji kutoka hekta 694,715 mwaka 2020 hadi hekta 983,466.06 mwaka 2024, kulikochangiwa na ongezeko la miradi ya umwagiliaji kutoka 13 mwaka 2020 hadi 780 mwaka 2025.

- Kukamilika kwa ujenzi wa maghala 46 na vihenge 20 vyenye uwezo wa kuhifadhi mazao tani 219,921 na hivyo kuchangia juhudi za Serikali za kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno.

# SEKTA YA UJENZI NA USAFIRI NA USAFIRISHAJI

- Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025 Sekta ya ujenzi imewezesha usafiri na usafirishaji kupitia ujenzi na kukarabati miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo barabara na madaraja, viwanja vya ndege na majengo mbalimbali.
  - Kuongezeka kwa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka kilomita 38,086.95 mwaka 2020 hadi 40,902.434 mwaka 2025
  - Kuongezeka kwa mtandao wa barabara za changarawe kutoka kilomita 24,493 mwaka 2020 hadi 44,372.21 mwaka 2025.
  - Kukamilisha ujenzi wa madaraja kumi (10) ya Gerezani (Dar es Salaam), Tanzanite (Dar es Salaam), Wami (Pwani), Kitengule (Kagera), Kiyegeya (Morogoro), Ruaha (Morogoro), Ruhuhu (Ruvuma), Mpwapwa (Dodoma), Msingi (Singida) na JP Magufuli (Kigongo – Busisi).



# SEKTA YA UJENZI NA USAFIRI NA USAFIRISHAJI…2



- Kukamilika kwa awamu ya pili kilomita 20.3 ya mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) (Mbagala - Mzunguko wa Bandari (Bendera Tatu), Bendera Tatu – Kariakoo, Sokoine – Zanaki, Barabara ya Kawawa – Barabara ya Morogoro (Magomeni) pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu, kilomita 23.3 kutoka katikati ya Jiji hadi Gongo la Mboto ambao umefikia asilimia 80 na awamu ya nne, kilomita 30.1 kutoka katikati ya Jiji hadi Tegeta

- Ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami ya Mzunguko wa Nje (Outer Ring Road) katika Jiji la Dodoma

- Upanuzi wa Barabara Kuu ya TANZAM sehemu ya Uyole – Ifisi – Songwe Airport Jijini Mbeya yenye urefu wa kilomita 36 kutoka njia mbili kuwa njia

# SEKTA YA UJENZI NA USAFIRI NA USAFIRISHAJI…3

- Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa unaohusisha ukarabati na uboreshaji wa barabara ya kuruka na kutua ndege (Runway), ujenzi wa maegesho ya ndege (Apron), barabara za viungio (taxiway), jengo la zimamoto, jengo la kuongozea ndege na usimikaji wa taa za kuongozea ndege na taa za usalama.
- Ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Tabora, Kigoma, Geita ukarabati wa viwanja vya ndege vya Musoma, Sumbawanga, Shinyanga Arusha, Songea, Mpanda, Kahama na Mtwara.
- Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato – Dodoma.
- Ujenzi wa vivuko vipya sita (6) vya Mafia – Nyamisati, Bwiro – Bukondo, Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Nyakaliro – Kome na Buyagu – Mbalika.



# SEKTA YA UJENZI NA USAFIRI NA USAFIRISHAJI…4



- Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha Dar es Salaam – Makutupora (km. 722) na vipande vingine vya kuunganisha reli ya kisasa ya SGR vya Mwanza - Isaka (km 341), Makutupora – Tabora (km 368), Tabora – Isaka (km 165), Tabora – Kigoma (km 506), na Uvinza - Malagarasi - Musongati (Km 282).

# SEKTA YA UJENZI NA USAFIRI NA USAFIRISHAJI…5



- Maboresho ya miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam ambayo yalihusu uboreshaji wa gati Na. 1 – 7, kuchimba kina cha maji kutoka mita 11 hadi mita 14.5 na upanuzi wa lango la kuingilia na kugeuzia meli, ujenzi wa gati maalumu (RoRo berth) la kuhudumia meli za magari na eneo la kuegesha magari

- Maboresho ya Bandari ya Tanga kwa kufanya ukarabati wa gati namba 1 na 2 zenye urefu wa mita 300, ununuzi wa mitambo na kuongeza kina kutoka mita 3 hadi 13.

- Ujenzi wa gati, uzio wa bandari na barabara inayounganisha gati jipya na maeneo mengine katika Bandari ya Mtwara; na

- Ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala.

# SEKTA YA UJENZI NA MAWASILIANO YA SIMU

- Kuongeza minara ya mawasiliano kutoka minara 754 mwaka 2020 hadi 9,278 mwaka 2025 na hivyo kuongeza wigo wa upatikanaji wa mawasiliano kwenye maeneo yenye changamoto.



# SEKTA YA UJENZI NA NISHATI



# SEKTA YA UJENZI NA NISHAT…2

- Kukamilisha ujenzi wa miradi ya kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115;

- Mradi wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I Extension MW 185 kwa kutumia Gesi Asilia,

- Mradi wa Rusumo ambao umetekelezwa katika Mto Kagera kwa ushirikiano wa nchi tatu za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa wa umeme (MW 26.67).

- Kukamilisha miradi ya usambazaji umeme ikiwemo mradi wa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme yenye urefu wa kilomita 414 kutoka Singida - Arusha - Namanga (kilovoti 400),



# SEKTA YA UJENZI NA NISHAT…3




- njia yenye urefu wa kilomita 144 kutoka Geita – Nyakanazi (kilovoti 220),
- njia ya kutoka Julius Nyerere hadi Chalinze (kilovoti 400/220/132);
- njia kutoka Nyakanazi hadi Kigoma (kilovoti 400);
- njia yenye urefu wa kilomita 115 kutoka Tabora - Urambo (kilovoti 132),
- njia yenye urefu wa kilomita 94 kutoka Rusumo-Nyakanazi (kilovoti 200), na
- njia ya kusafirisha umeme kwenye njia ya reli (Standard Gauge Railway – SGR - kilovoti 220).

# SEKTA YA UJENZI NA DIRA 2050

**Lengo Na. 1: Uchumi wa Kipato cha Kati Ngazi ya Juu, Ulio Mseto, himilivu, Jumuishi na Shindani.**

| Shabaha | Mahitaji ya Miundombinu Jengwa |
|---|---|
| Nchi ya kipato cha kati ngazi za juu unofikia thamani za dora za kimarekani trilioni moja, na wastani wa pato la mtu mmoja lenye thamani ya dola za Marekani 7,000 kwa mwaka. | Miundombinu ya kiuchumi katika sekta zote za uzalishaji |
| Kutokomeza umaskini uliokithiri kwa makundi yote. | Miundombinu na makazi bora, maji safi na salama, elimu, nishati safi, kilimo na umwagiliaji, usafiri na usafirishaji, masoko, n.k. |
| Kuwa mzalishaji mkuu wa chakula barani Afrika na miongoni mwa nchi kumi bora duniani. | Kilimo na umwagiliaji, maghala, usafiri na usafirishaji, miundombinu ya ufugaji na uvuvi, mawasiliano |

# SEKTA YA UJENZI NA DIRA 2050

## Lengo Na. 2: Maisha bora na ustawi kwa wote

| Shabaha | Mahitaji ya Miundombinu Jengwa |
|---|---|
| Mtanzania anaishi kwa wastani wa miaka 75, akifurahia maisha bora na afya njema. | Miundombinu ya makazi bora, maji safi na salama, nishati safi, afya bora, elimu, kilimo na umwagiliaji, maghala, n.k |
| Watoto wote wa kike na wa kiume wanapata malezi na makuzi bora ya | Miundombinu ya makazi bora, elimu, maji safi, afya bora, nishati safi, usafiri na usafirishaji, n.k. |
| Kutokomeza vifo vya wajawazito, Watoto wachanga na Watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano. | Miundombinu ya kutolea afya bora, maji safi na salama, kilimo na umwagiliaji, usafiri na usafirishaji, elimu bora, nishati safi, n.k. |

# SEKTA YA UJENZI NA DIRA 2050

## Lengo Na. 2: Maisha bora na ustawi kwa wote...2

| Shabaha | Mahitaji ya Miundombinu Jengwa |
|---|---|
| Huduma bora za afya kwa wote | Majengo ya kutolea huduma za afya bora |
| Mfumo bora na jumuishi wa elimu na mafunzo katika ngazi zote. | Majengo ya shule na vyuo vya ngazi zote |
| Watoto wote wa kike na wa kiume wana fursa sawa za kupata elimu ya awali yenye kujenga msingi imara kwa ajili ya kujifunza na kujielimisha bila ukomo. | Majengo ya shule za awali za msingi |
| Watanzania wote wanapata elimu msingi bora na angalau asilimia 25 wanapata elimu ya juu. | Majengo ya shule za awali za msingi |
| Upatikanaji wa huduma jumuishi za hifadhi ya jamii kwa wote. | Majengo ya ofisi, vitega uchumi |

# SEKTA YA UJENZI NA DIRA 2050

## Lengo Na. 2: Maisha bora na ustawi kwa wote...3

| Shabaha | Mahitaji ya Miundombinu Jengwa |
|---|---|
| Upatikanaji sawia wa maji safi na salama, huduma za usafi wa mazingira na nishati safi | Miundombinu ya maji safi na salama, usafi wa mazingira |
| Angalau asilimia 50 ya Watanzania wana ajira zenye staha katika sekta rasmi. | Fursa za ajira katika miradi ya ujenzi, |
| Kuongezeka kwa matumizi ya nishati ya umeme kufikia wastani kwa mwaka 3,000KWh kwa kila mtu | Miundombinu ya nishati safi na salama |
| Tanzania kuwa kinara barani Afrika na miongoni mwa nchi kumi bora duniani katika kupunguza pengo la kijinsia kwa angalau asilimia 85. | Miundombinu yote ya kiuchumi na kijamii |

# SEKTA YA UJENZI NA DIRA 2050

## Lengo Na. 3: Taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija, na linalostahimili mabadiliko ya tabia nchi

| Shabaha | Mahitaji ya Miundombinu Jengwa |
|---|---|
| Kuwa na viwango vya juu vya uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na kuifanya Tanzania kuwa kati ya nchi kumi bora barani Afrika. | Miundombinu yote ya kijamii na kiuchumi iliyosanifiwa na kujengwa kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabia nchi. |

# SEKTA YA UJENZI NA DIRA 2050

**Lengo Na. 4: Jamii yenye umahiri na ujuzi wa kutumia teknolojia za kidijitali katika kuchochea ubunifu na kuongeza ushindani wake kimataifa.**

| Shabaha | Mahitaji ya Miundombinu Jengwa |
|---|---|
| Jamii yenye umahiri wa kidijitali, ambapo angalau asilimia 70 ya wananchi wanatumia TEHAMA. | Miundombinu ya Tehama |
| Zaidi ya asilimia 80 ya huduma za serikali zinapatikana kupitia mifumo ya kidijitali salama na jumuishi. | Miundombinu ya Tehama |


ASANTE SANA